**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne . Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Tume ya kukabiliana na ufisadi ___1___ kufanya uchunguzi wa kina kuhusu ___2___ wa pesa katika wizara ya afya. Ni jambo la ___3___ kuona kuwa ufisadi hapa nchini ___4___ umekuwa dondandugu. Wanasiasa nao wanaombwa ___5___ siasa katika suala ___6___ .Wote wafyate ndimi ___7___ na kuacha mkondo wa sheria kutamalaki.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. imekata kauli | B. imekata kamba | C. imetia shime | D. imepiga konde la nyuma |
| 2. | A. uvujaji | B. ufujaji | C. uvunjaji | D. uvimbaji |
| 3. | A. kutia moyo | B. kuuma uzi | C. kuvunja moyo | D. kulia ngoa |
| 4. | A. mwetu | B. yetu | C. kwetu | D. petu |
| 5. | A. wasiingie | B. wasiigize | C. wasiingiliwe | D. wasiingize |
| 6. | A. huu | B. hiki | C. hii | D. hili |
| 7. | A. lao | B. wao | C. zao | D. yao |

Potovu alipofikishwa mahakamani ___8___ tuhuma za wizi, alijaribu kuzua fujo. Papo hapo ___9___ kilimvisha pingu mikononi na kumwamuru asimame ___10___ ili asomewe mashtaka ___11___ . Hakimu alimfahamisha makosa yake ___12___ potovu alikataa katakata. Hapo kesi yake ___13___ naye akaamuliwa awekwe rumande na asubiri majuma ___14___ .Mwishowe alifungwa kwa kupatikana na mali ya wizi. Naye ___15___ .

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 8. | A. na | B. kwa | C. ya | D. za |
| 9. | A. kikosi cha askari | B. kizio cha askari | C. kilinge cha askari | D. kishuke cha askari |
| 10. | A. kortini | B. handakini | C. kizimbani | D. magofuni |
| 11. | A. yake | B. lake | C. zake | D. zao |
| 12. | A. na | B. wala | C. bali | D. hata |
| 13. | A. iliahirishwa | B. ilihairishwa | C. ilihamishwa | D. iliinuliwa |
| 14. | A. mbili | B. tatu | C. tano | D. sita |
| 15. | A. mpanda ngazi hushuka | B. Mkamatwa na ngozi ndiye mwizi | C. Mwana umleavyo ndivyo akuavyo | D. Mwizi akishikwa husema akaonewa |



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**Kutoka swali nambari 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo.**

16. Jina 'chakaramu' lina silabi ngapi?
A. 4 B. 8 C. 9 D. 2

17. **Chagua sentensi inayoonyesha hali timilifu**
A. Ungalikuja mapema ungalinikuta
B. Atazichunguza hali zote
C. Naelekea ng'ambo kwa masomo zaidi
D. Dada ameenda kwa shangazi yake

18. Chagua sentensi yenye kivumishi halisi
A. Mkulima alilima shamba lote akalimaliza fyu!
B. Magari mazuri huwa ni ya bei nafuu
C. Akumlikaye mchana usiku atakuunguza
D. Wote wachezeao tope huwarukia

19. Tunasema mjanja kama:-
A. Sungura B. Kobe
C. Nyani D. Kondoo

20. **Chagua sentensi iliyotumia kiashiria kisisitizi**
A. Magonjwa haya haya yatapata tiba
B. Shuleni kule kule kumepandwa minazi
C. Huyo ndiye mlevi aliyekamatwa jana
D. Zizi lili hili litajengwa upya

21. Chagua pambo ambalo huvaliwa mguuni.
A. Kikuba B. Bali
C. Furungu D. Kidani

22. **Andika kwa wingi**
Ganda la muwa jana chungu akaona kivuno
A. Maganda ya miwa ya jana vyungu huona kivuno
B. Maganda ya miwa ya jana vyungu wakaona kivuno
C. Maganda ya miwa jana chungu wakaona kivuno
D. Maganda ya miwa jana chungu wakaona vivuno

23. **Kanusha sentensi ifuatayo**
Mashimo yaliyochimbwa yatapandwa miti
A. Mashimo ambayo hayakuchimbwa hayatapandwa miti
B. Mashimo yaliyochimbwa hayakupandwa miti
C. Mashimo yaliyochimbwa hayatapandwa miti
D. Mashimo yasipochimbwa hayatapandwa miti

24. Mtoto wa simba huitwaje?
A. Simba marara B. Shibli
C. Simba buka D. Kitungule

25. Maneno asteaste, haraka, kwa sauti, kijeshi ni mifano ya:-
A. Vivumishi B. Vitenzi
C. Vielezi D. Viwakilishi

26. $^{3}/_{7}$ kwa maneno ni:-
A. Subui tatu B. Tusui tatu
C. Theluthi tatu D. Sudusi tatu

27. Chagua sentensi yenye dhana ya masharti
A. Usipoziba ufa utajenga ukuta
B. Magonjwa hayajakuwa yakitibiwa vilivyo
C. Kauleni huwa hasumbui studioni
D. Wasingeny'ang'anywa silaha wangekuwa washindi

28. Chagua sentensi iliyotumia - na- ya kuonyesha ufupishaji wa nafsi?
A. Rehema ana kabuti jipya
B. Wenyeji walielekezwa na wageni
C. Matunda na mboga ndivyo vyakula muhimu
D. Naye alicheza ngoma hiyo vizuri sana

29. Chagua sentensi yenye 'kwa' ya akisami
A. Wageni wetu walisafiri kwa garimoshi la kisasa
B. Mama ndiye aliyetembea na baba sako kwa bako
C. Waliofika mkutanoni walikuwa watano kwa tisa
D. Chesoni alitembea kwa haraka ili amfikie ninaye

30. **Tambua umbo hili.**



A. Nyoka B. Parafujo
C. Mshazari D. Wimbi



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali nambari 31 - 40 .**

Katika kijiji cha Madongo paliishi msichana aliyeitwa Ringo. Alikuwa msichana mwenye kiuno cha nyigu na urembo wa hurulaini. Kusema ukweli alikuwa ameumbwa akaumbika. Ila ya familia yake ilikuwa ukata. Walikuwa maskini ambao hawakuwa na mbele wala nyuma. Kutokana na ufukara huu mashaka yaliwaandama moja baada ya jingine. Hata hivyo wazazi wake Ringo <u>hawakwenda nguu</u>. Walivunja mgongo ili Ringo apate lishe, mavazi na elimu . Ninakumbuka vizuri namna baba yake Ringo alivyorauka kabla ya jogoo wa kwanza kuwika na kurudi nyumbani baada ya giza la kaniki kufunika ulimwengu mzima. Kulonga mithaki mtoto ni kito mzigo mzito.

Ringo alikua na kuwa mwenye mwili na maungo ya kupendeza . Kwa nyota ya jaha, alikuwa mtoto mwenye akili zake. Kwa weledi wake na ukakamavu wake masomoni aliondokea kupendwa na kuenziwa na watu wote si shuleni si nyumbani. Wanakijiji pamoja na majirani walisikika mara kwa mara wakijifaragua namna walivyokuwa na binti mrembo duniani. Ringo alisoma hadi upeo wa masomo. Wahenga walisema kuwa elimu ni bahari isiyofika mwisho na ni hazina isiyoweza kutekwa na mahasimu.

Huko chuoni alisomea uwakili. Akawa akiporomosha Kiingereza kuliko Mwingereza mwenyewe .Ajabu huajabiwa. Hii ni kwa sababu Ringo alipopata mfuko mzito hakuwahi kuwatembelea wazazi wake ambao walikuwa wakigugunwa na umaskini kijijini. Hata hivyo wazazi wake walipopatwa na shida aliwapiga jeki kwa kuwatumia msaada waliouhitaji. Shida ni kuwa Ringo alikula yamini kutokanyaga mashambani bilikuli. Usisahau hata kwa marafiki zake alijitambulisha kama aliyezaliwa mjini na alipoulizwa kuhusu wazazi wake alisema kuwa walikuwa wameaga dunia. Ati yeye alikuwa mwanamkiwa. Ajabu iliyoje! Kumbe hakuna kizuri kisicho na dosari.

Wazazi wake Ringo waliingiwa na wasiwasi. Hawakuwa na habari namna Ringo alivyokuwa akiendelea mjini. Kwa kuwa damu ni nzito kuliko maji, baba yake Ringo aliamua kufunga safari kuelekea mjini kumwona mwanawe. Alimtafuta mzee mmoja jirani aliyejua makao ya Ringo. Baba yake Ringo alipofika mjini alipatana na mtoto wake wa pekee na kuwa na furaha ghaya.Mambo ni kangaja huenda yakaja. Ringo alimkemea na kumkaripia kwa huo ujio wake ambao hakuutarajia wala kuufahamu. Babake aliomba radhi ya kutaka kuondoka na kurejea mashambani maadamu mtoto wake alikuwa salama salmini na mwenye afya.

Siku iliyofuata kabla ya babake kuondoka, marafiki zake Ringo walifika nyumbani kwake wakimtaka waende kupunga unyunyu. Hapo ndipo walipomhoji kumhusu baba yake waliyemuona. Hapo Ringo aliwapaka mafuta kwa mgongo wa chupa kuwa alikuwa mzee aliyekuwa amepiga chechele. Usisahau kuwa baba yake Ringo aliyasikia maneno yao yote kuanzia alfa hadi Omega. Aliungulika moyoni asielewe sababu ya Ringo kumkana. Baadaye, baba yake waliondoka na kuelekea nyumbani. Alipokuwa akirudi kwao, aligongwa dafrau na gari na akafa fofofo.

Ringo aliporudi hakuamini alipopata habari hizo. Wenzake walifika kujua mbona alikuwa akilia naye bila kuchelea aliwapasulia mbarika. Wote walibaini kuwa Ringo hakuwapenda wazazi wake. Hapo ndipo walipomwambia kuwa hata <u>yeye angefanyiwa vivyo hivyo baada ya kuzeeka.</u> Ni vizuri tuwaheshimu wazazi wetu wakati wowote , Hata wakiwa wazee

31. Wazazi wa Ringo :-
    A. Walimtelekeza mwana wao kwa kumnyima mahitaji yake ya kila siku
    B. Walimlea mwana wao kwa kumwengaenga kama yai lililovunjika
    C. Walimlea mwana wao kwa kujitolea na kumkidhia mahitaji yake ya kimsingi
    D. Walikuwa matajiri waliojulikana karibu na mbali

32. Ni nini maana ya <u>'Hawakwenda nguu'</u> kulingana na kifungu?
    A. Hawakufurahia
    B. Hawakupoteza matumaini
    C. Hawakushtushwa
    D. Hawakukubaliana

33. Ringo hakutaka kujulikana asili yake kwa kuwa:-
    A. Alichelea kuaibika
    B. Miaka mingi aliishi mjini
    C. Alikuwa amesahau alikozaliwa
    D. Marafiki zake hawakuwapenda watu wa mashambani

34. Kutoka aya ya pili, Ringo amejitokeza na sifa zipi?
    A. Mzembe, mbinafsi na mpole
    B. Mchapakazi, mwenye maringo na mkakamavu
    C. Mwenye maringo, mwongo na mkakamvu
    D. Mrembo, mwerevu na mkakamavu

35. Babake Ringo alijuanje alikoishi bintiye?
    A. Alielekezwa na jirani kisha akajiendea mjini
    B. Alikuwa na ramani aliyopewa na bintiye
    C. Aliongozwa na jirani aliyejua alikokuwa Ringo
    D. Alikisia tu kwa kuwa mjini alikujua sana



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

36. Ni nini hasa kilichomfanya Ringo kumkemea baba yake?
A. Baba yake alimtembelea bila kukata notisi ya ujio wake
B. Tayari Ringo alikuwa amewaelezea marafiki zake kuwa hakuwa na wazazi
C. Alijua kuwa angegharamika sana kuwapokea wageni wawili ambao wangekaa kwa muda mrefu.
D. Alihofia kuonyesha picha yake halisi

37. Kwa nini mwandishi anasema kuwa mambo ni kanganja huenda yakaja?
A. Alidhania kuwa furaha aliyokuwa nayo ingezimwa na mwanawe
B. Hakutarajia baba yake Ringo apokee makaribisho ya hadhi kuu
C. Licha ya kuwa baba yake Ringo alikuwa na hamu ya kumwona bintiye, mambo yalienda kinyume
D. Kwa kuwa mambo yalienda jinsi yalivyopangwa

38. 'Akawa akiporomosha Kiingereza kuliko Mwingereza mwenyewe. Hii ni tamathali gani?
A. Chuku B. Kinaya
C. Tashbihi D. Istiara

39. Baba yake Ringo aliungulika ndani kwa ndani kwa kuwa:-
A. Hakujua mwana wake alikuwa ameenda wapi
B. Hakutarajia mwana wake amkane
C. Hakujua hali ya afya ya mwana wake
D. Mwana wake alikuwa akiishi maisha ya hali ya chini

40. Yeye angefanyiwa vivyo hivyo baada ya kuzeeka
Ni methali gani ambayo inalenga kauli hii?
A. Kilichompata peku hata na lungo ni kicho
B. Lila na fila havitangamani
C. Aliye juu mngojee chini
D. Mwana mtukana nina kuzimu enda kiona.

**Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali nambari 41 - 50 .**

Asasi zisizo za kiserikali zina dhima kuu sana zinazotekeleza humu nchini mwetu. Ni maendeleo mengi sana yaliyoafikiwa kutokana na asasi hizi. Ni dhahiri shahiri kuwa maendeleo mengi ambayo tunanjivunia kama jamii hasa katika sehemu za mashinani; yametekelezwa na asasi hizi. Miradi mingi ikiwemo juhudi za kupambana na makali ya ugonjwa wa ukimwi, maji ya kunywa, kilimo, ufadhili wa kimasomo na kadhalika, uhifadhi wa mazingira yote imewezekana kwa jitihada za asasi hizi zisizo za kiserikali.

Waswahili husema kuwa hakuna kapa lisilo na usubi. Uchunguzi unaonyesha kuwa ingawa mashirika haya yanajivunia kutekeleza mengi, maendeleo ni machache sana ikilinganishwa na kiasi cha pesa ambacho kimetolewa na wafadhili. Madai yaliyotolewa na wanaharakati wa kutetea haki za kibinadamu humu nchini majuma kadhaa yaliyopita kuwa walaghai wa kitaalamu wameingilia sekta hii kuwapora wafadhili pesa zao yana ukweli fulani. Kumbuka lisemwalo lipo na kama halipo laja.

Kuna mbinu kadhaa ambazo hutumiwa na mashirika haya katika uporaji huu. Njia ya kwanza ni kupitia uandishi wa mapendekezo ya miradi isiyokuwepo. Mengi ya mapendekezo haya huandikwa kwa lugha ya mvuto kuwashawishi wafadhili watoe pesa zao. Kuna uwezekano umewahi kukutana na wasomi waliobobea katika taaluma ya kuandika miradi kwa malipo. Hao ndio wajuao mambo ya kujumuishwa kwenye mapendekezo ya miradi ili kuwateka wafadhili. Kile wafanyacho ni kuandika mapendekezo na baadaye hupewa sehemu yao ya pesa hizo punde zinapotolewa.

Njia nyingine sio wizi wa wazi kwani huhusisha matumizi ya pesa kwa njia ambazo hazikukusudiwa. Badala ya kutumiwa fedha za wafadhilil kutekeleza miradi ya maendeleo iliyopendekezwa, baadhi ya wasimamizi wa mashirika haya huweka pesa mifukoni mwao.

Kuna viongozi wengine wa mashirika hayo ambao hutumia ufadhili huo kuzuru mataifa ya kigeni kwa kusingizia kuhudhuria makongamano ya kukata na shoka katika hoteli kubwakubwa nchini. Kinaya kilichoje ni kuwa pesa zilizotafutwa kuwasaidia wajane katika vitongoji vya mashambani zinatekeleza miradi bandia mijini. Inasemekana baadhi ya miradi ya mashirika hutekelezwa kimaandishi tu na maafisa wanaosimamia mashirika haya bila kuwahusisha walengwa.

Zaidi ya yote, asasi hizi kuna zile hutumia pesa nyingi katika masuala ya utawala na usimamizi badala ya miradi ya maendeleo. Mashirika haya ni muhimu nchini. Hata hivyo hayana budi kusimamiwa na watu wenye maono ili kuyaafikia malengo yao.

Ushauri wangu ni kuwa, utumizi mbaya wa mali ya umma lazima ukome mara moja. Watu wazoee kula jasho lao. Kwa kufanya hivi, maendeleo yatagonga kona zote za nchi. Wafanyakazi waache tamaa ya kupata mali kwa njia za mkato.



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**41.** Ni wazi kuwa:-
A. Asasi zisizo za serikali zimefanya mengi kuliko serikali yenyewe
B. Mwafaka wa maendeleo hutegemea serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali
C. Dhima kuu ya kuhakikisha kuwa kuna maendeleo ni ya asasi zisizo za kiserikali
D. Wananchi wote wameelewa kuwa kwa njia moja au nyingine wamewahi kusaidiwa na mashirika yasiyo ya kiserikali

**42.** Zifuatazo ni dhima za asasi zisizo za kiserikali ila:-
A. Kuhakikisha watoto wote maskini kwa tajiri wanasoma
B. Kueneza maji safi na salama ya kutumiwa
C. Kutoa dawa za kupunguza makali ya ugonjwa wa ukimwi
D. Kuwafaa wanafunzi wasio na uwezo wa kuyamudu masomo.

**43.** Ni nini <u>hasa</u> kimeathiri utendakazi wa asasi zisizo za kiserikali?
A. Pesa
B. Miradi mingi
C. Ujeuri
D. Tamaa

**44.** Ni kweli kuwa:-
A. Asasi hizi zisizo za kiserikali hazijatekele za mambo muhimu nchini.
B. Wafadhili kwa sasa wamedinda kugharamia shughuli za mashirika haya.
C. Mali yaliyotumiwa vibaya ni mengi kuliko yaliyotumika vilivyo
D. Wakuu wa serikali ndio wanaofuja mali ya mashirika yasiyo ya kiserikali.

**45.** Jina <u>***'wafadhili'***</u> limetumika sana katika kifungu . Lina maana gani?
A. Waingereza
B. Watoa msaada
C. Wapokezi wa msaada
D. Wakuu wa idara

**46.** Kulingana na misimamo ya wanaharakati wa kutetea haki za kibinadamu
A. Asasi zisizo za kiserikali hazina uzito wowote humu nchini
B. Viongozi wa asasi zisizo za kiserikali wamejukumika vilivyo
C. Baadhi ya viongozi wa asasi hizi ni walaghai
D. Hakuna asasi nzuri iwayo gani bora tu si ya kiserikali

**47.** Chagua kauli iliyo sahihi:-
A. Ufisadi huwa ni baina ya wanaotoa misaada na walioandika mapendekezo
B. Msimulizi ndiye aliyesaidia katika kutafuta wajuzi wa kuandika miradi
C. Hakuna mradi wowote wa pembe za chaki ambao umewahi kugunduliwa
D. Wanaosimamia miradi huhusika katika ulaghai wa kuandikiwa miradi

**48.** Pesa za wafadhili zafaa kutumiwa katika :-
A. Kulipa mishahara minono kwa wote walioshiriki katika ufisadi
B. Kuhudhuria semina za kujiimarisha kitaaluma ili kuafikia malengo ya mradi wowote ule
C. Kuzuru mataifa mengi ya Ulaya ili kusoma utendakazi wao
D. Kuwasomesha watoto wa viongozi wa asasi zisizo za kiserikali

**49.** Kulingana na msimulizi
A. Asasi zisizo za kiserikali ni muhimu sana
B. Mashirika yasiyo ya kiserikali si muhimu
C. Hajui iwapo mashirika haya ni muhimu au la
D. Mashirika yote yasiyo ya kiserikali ni mabaya

**50.** Kulingana na aya ya mwisho:-
A. Watawala waadilifu watafanikisha juhudi za asasi zisizo za kiserikali
B. Umoja wa wananchi utakomesha maovu yote yanayoendelea nchini
C. Wafadhili wanafaa kusitisha shughuli zote za kusaidia asasi zisizo za kiserikali
D. Dola limeacha uongozi wa nchi mikononi mwa mashirika yasiyo ya kiserikali.



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com